



12

KIBABII UNIVERSITY

UNIVERSITY EXAMINATIONS

2019/2020 ACADEMIC YEAR

SECOND YEAR SECOND SEMESTER

MAIN EXAMINATION

DIPLOMA IN EDUCATION (ARTS)

COURSE CODE: EDK 108

COURSE TITLE: UTANZU WA USHAIRI

DATE: 9-11-2020

TIME: 9:00am-11:00am

MAELEKEZO

- i. Jibu maswali **matatu** pekee
- ii. Swali la **KWANZA** ni la **LAZIMA**
- iii. Usiandike chochote kwenye karatasi hii ya maswali

Muda: Saa Mbili (2)

KIBU observes **ZERO** tolerance to examinations cheating

Maswali

1. a) Fafanua kwa tafsili dhana ya ushairi. (alama 5)
 - b) Kwa kurejelea hoja zozote tano, tofautisha ushairi wa kimapokeo na ushairi huru. (alama 5).
 - c) Pambanua umuhimu wa ushairi katika jamii ya kisasa. (alama 10).
 - d) Kwa kutolea mifano mwafaka, taja na ueleze vipengele vyatuhuru wa mshairi (alama 10).
2. Eleza mambo matano yanayozingatiwa katika uchambuzi wa bahari katika shairi. (alama 20).
3. Fafanua asili na historia ya ushairi katika kipindi cha utasa na katika kipindi cha sasa (alama 20).
4. Soma shairi lifuatato kisha ujibu maswali uliyopewa. (alama 20).

Niokoe muokozi, unondolee mashaka
Kuyatukua siwezi, mjayo nimedhikika
Nimekithiri simanzi, ni katika kuudhika
Mja wako nasumbuka, nipate niyatakayo

Mja wako nasumbuka, nataka kwao afua
Nirehemu kwa haraka, nami nipate pumua
Naomba hisikitika, na mikono hiinua
Mtenda ndiwe moliwa, nipate niyatakayo

Mtenda ndiwe moliwa, we ndiwe Mola anga
Mazito kuyaondoa, pamoja kuyatenga
Ukauepusha ukiwa, ya pingu zilizonifunga
Nikundulia muwanga, nipate niyatakayo

Muwanga nikundulia, nipate toka kizani
Na huzuni n'ondolea, itoke mwangu moyoni
Mambo mema niegeshea, maovu nisitamani
Nitendea we Manani, nipate niyatakayo

Igeuze yangu nia, dhaifu unipe mema
Nili katika dunia, kwa afia na uzima
Moliwa nitimizia, yatimize yawe mema
Nifurahike mtima, nipate niyatakayo

Maswali

- a. Shairi hili ni sala kwa Mungu. Thibitisha (alama 4)
 - b. Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa mshairi kwa kurejelea ubeti wa 5. (alama 4)
 - c. Bainisha toni ya shairi hili. (alama 2)
 - d. Changanua sifa za kiarudhi za ubeti wa tano (alama 4)
 - e. Eleza bahari za kishairi zinazojitokeza. (alama 2)
 - f. Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)
5. Ukiirejelea hoja tano, bainisha mambo yanayochangia kuwepo kwa mgogoro wa ushairi. (Alama 20).